# HALMASHAURI YA MJI KASULU

***(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi wa Mji)***

***Simu:*** *+255282810335*
***Tovuti:***[*www.kasulutc.go.tz*](http://www.kasulutc.go.tz)
***Baruapepe:***[*td@kasulutc.go.tz*](mailto:td@kasulutc.go.tz)

*UnapojibuTafadhaliTaja:*

Ofisi ya Mkurugenzi wa Mji
Halmashauri ya Mji Kasulu
S. L. P 475,
**KASULU.**

***KUMB NA.KSTC/I.2/9/25***

***24/05/2022***

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Halmashauri ya Mji Kasulu imepokea kibali cha ajira kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kufuatia kibali hicho Mkurugenzi wa Mji wa Kasulu anawatangazia watanzania wote wenye sifa na uwezo wa kutuma maombi ya nafasi hizo kwa kuzingatia sifa, vigezo na maelekezo yaliyo katika tangazo hili.

### 1. MTENDAJI WA MTAA III (NAFASI 36)

**Sifa za Mwombaji**

- Cheti cha Kidato cha IV au VI
- Aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na sayansi ya sanaa kutoka chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo-Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

**Kazi za Kufanya:-**

1. Mratibu na Mtekelezaji wa sera na sheria zinazotekelezwa naHalmashauri katika Mtaa.
2. Mshauri wa Kamati ya Mtaa kuhusu mipango ya Maendeleo katika Mtaa.
3. Mshauri wa Kamati ya Mtaa kuhusu masuala ya Ulinzi na Usalama.
4. Msimamizi wa utekelezaji wa mikakati mbalimbali inayohusu uondoaji wa njaa na umaskini katika Mtaa.
5. Kusimamia Ukusanyaji wa Mapato ya Halmashauri na kutunza kumbukumbu za walipa kodi wote.
6. Kuandaa na kutunza rejesta ya wakazi wote wa Mtaa.
7. Kusimamia Utungaji na utekelezaji wa sheria ndogo ndogo za mitaa.
8. Kutekeleza majukumu mengine kadri atakavyopangiwa na Mwajiri wake.

**MSHAHARA**

Kwa kuzingatia ngazi ya Mshahara kwa watumishi wa Umma **TGS $B_1$** kwa mwezi

**Masharti ya kazi**

Kazi ina masharti ya kudumu na malipo ya uzeeni.

## 2. DEREVA DARAJA LA II (NAFASI 4).

**Sifa za Mwombaji**

- Awe na Cheti cha Kidato cha IV
- Awe na Leseni daraja la E au $C_1$ ya uendeshaji wa magari
- Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji wa magari (basic driving course) yanayotolewa na chuo kinachotambuliwa na serikali
- Waombaji wenye cheti cha majaribio ya ufundi daraja la II, watafikiriwa kwanza

**Kazi za Kufanya:-**

1. Kuendesha magari ya abiria na malori
2. Kuhakikisha gari na vyombo vyake vipo katika hali nzuri wakati wote, na kufanya uchunguzi wa gari kabla na baada ya safari ili kugundua ubovu unaohitaji matengenezo
3. Kufanya matengenezo madogomadogo katika gari
4. Kutunza na kuandika daftari ya safari "Log-book" kwa safari zote
5. Na kazi nyingine atakazopangiwa na msimamizi wake

**MSHAHARA.**

Kwa kuzingatia ngazi ya Mshahara kwa watumishi wa Umma **TGS $B_1$** kwamwezi.

**Masharti ya kazi.**

Kazi ina masharti ya kudumu na malipo ya uzeeni.

## 3. KATIBU MUHTASI DARAJA LA III (NAFASI 3).

***Sifa za Mwombaji.***

- Awe na Cheti cha Kidato cha IV
- Awe ufaulu wa mafunzo ya uhazili kwa ngazi ya cheti cha Astashahada (certificate) kutoka chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC) au chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali
- Awe hajawahi kuajiriwa serikalini

***Kazi za Kufanya:-***

1. Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida
2. Kusaidia kupokea wageni, kuwasaili shida zao na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa

vikao, safari za mkuu wake na ratiba ya kazi zingine zilizopangwa kutekelezwa katika ofisi anamofanyia kazi kumuarifu Mkuu wake kwa wakati unaohitajika.

4. Kusaidia kutafuta na kumpatia mkuu wake majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo ofisini
5. Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa maofisa walio katika sehemu alipo kukusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika
6. Kusaidia kufikisha maelekezo ya Mkuu wako wa kazi kwa wasaidizi wake na pia kumuarifu kuhusu taarifa zozote anazopewa na wasaidizi hao
7. Kutekeleza kazi zozote utakazokuwa umepangiwa na msimamizi wako wa kazi

**MSHAHARA.**

Kwa kuzingatia ngazi ya Mshahara kwa watumishi wa Umma **TGS $B_1$** kwa mwezi.

***Masharti ya kazi.***

Kazi ina masharti ya kudumu na malipo ya uzeeni.

**MAMBO YA KUZINGATIA KWA WAOMBAJI**

1. Muombaji awe raia wa Tanzania na awe tayari kufanya kazi sehemu yoyote katika Halmashauri ya Mji Kasulu
2. Awe mwenye umri kati ya miaka 18-45
3. Barua ya muombaji ziambatishwe na nakala za vyeti vya Elimu, Taaluma, cheti cha kuzaliwa na Picha mbili (2) za rangi (Passport size) za hivi karibuni
4. Barua za maombi ziambatishwe na maelezo binafsi ya muombaji (CV)
5. Testimonials, Provisional results, statements of results, hati za matokeo za kidato cha nne **HAVITAKUBALIWA**
6. Waombaji waliosoma nje ya nchi waambatishe uthibitisho wa vyeti vyao kutoka Baraza la Mitihan-+
7. i la Taifa (NECTA)
8. Pia tangazo hili linapatikana kwenye tovuti ya Halmashauri ambayo ni; *www.kasulutc.go.tz*
9. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **6/6/2022** saa **9:30 Alasiri**

**Maombi yote yatumwe kwa Anwani ifuatayo;**

Mkurugenzi wa Mji,
Halmashauri ya Mji,
S.L.P 475
**KASULU.**

Imetolewa na;

Dollar R. Kusenge
**MKURUGENZI WA MJI**
**HALMASHAURI YA MJI KASULU**

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MJI
KASULU